



**HAZINA YA MSAADA YA  
COVID-19 YA WASHINGTON  
KWA MHAMIAJI**

# Msaada wa dharura wa COVID-19—na wahamiaji kwa wahamiaji.

Kama wahamiaji, tumefanya Washington kuwa nyumbani kwetu. Ikiwa wewe ni mhamiaji na unapitia wakati mgumu kwa sababu ya COVID-19, na hujafuzu kupata msaada wa serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira, hazina hii ni kwa ajili yako.

## **Hazina hii ni nini?**

Hazina ya msaada ya COVID-19 ya Washington kwa mhamiaji inatoa pesa za msaada za COVID-19 kwa wahamiaji ambao hawajafuzu kupata msaada wa serikali au bima ya mtu asiyekuwa na ajira. Ukituma maombi, unaweza pata dola elfu moja ambayo utapata mara moja na utatumiwa moja kwa moja (unaweza pata hadi dola elfu tatu kwa kila nyumba).

## **Inafanya kazi vipi?**

Unaweza tuma maombi kwa kutumia mtandao, kupitia simu, au kwa kutuma barua. Njia zote tatu zinapatikana kwa lugha kadhaa. Punde tu maombi yako yakikubaliwa, utapata malipo yako kupitia kwa hundi, kadi ya zawadi (Visa au Mastercard)

## **Ni nani anasimamia hazina hii?**

Hazina hii inasimamiwa na mashirika ya jamii ya Washington yanayoongozwa na wahamiaji—watu wao hao ndio walioitisha kuundwa kwa hazina hii. Hii ni pamoja na Mtandao wa mshikamano wa wahamiaji wa Washington (WAISN), Mradi wa haki za wahamiaji wa kaskazini magharibi, na mashirika mengine mengi. Pesa zinatolewa na idara ya jamii na huduma za afya ya jimbo la Washington.

## **Je! Habari yangu iko salama?**

Ndio. Hakuna chochote katika maombi yako ambacho kitasambazwa kwa hiari kwa serikali, ICE, au watekelezaji wa sheria.

## **Ni nani anaweza tuma maombi kwa hazina?**

Ili kutuma maombi ya hazina ya msaada, ni lazima:

- Uwe unaishi katika jimbo la Washington
- Uwe na angalau umri wa miaka kumi na nane
- Uwe umeathirika kwa kiasi kikubwa na tandavu hii (kama vile kupoteza kazi, uwe umeambukizwa na virusi, au unamtunza mtu wa familia aliyeambukizwa na virusi)
- Usiwe unafaa kupata hazina ya msaada ya serikali au bima kwa asiyekuwa na kazi kwa sababu ya hali ya uhamiaji

Ukituma maombi, utahitajika kuonyesha nakala za baadhi ya stakabadhi ili kuonyesha utambulisho wako na unakoishi (kama vile kadi ya kitambulisho, bili ya matumizi, au risiti ya kodi ya nyumba).

## **Je! Sheria ya malipo ya umma itatumika?**

La. Hazina hii inachukuliwa kama msaada wa wakati mmoja kwa sababu ya janga na haifai kukuzuia kupata visa au kadi ya kijani siku za usoni.


**TUMA MAOMBI  
KUFIKIA DISEMBA  
TAREHE 6:**

**[www.immigrantreliefwa.org](http://www.immigrantreliefwa.org)**

**1-844-724-3737**

**(Jumatatu-ijumaa saa tatu  
asubuhi hadi saa tatu usiku)**

**Wahamiaji wanaotunzana.**



Inasaidiwa na kufadhiliwa na Idara ya Jamii na Huduma ya Afya ya jimbo la Washington.